*JARIDA LA CHALUFAKITA*
*Juz. 4, 2022, 51-64*

# NAFASI YA HADITHI KATIKA UKUZAJI WA STADI ZA KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA: MFANO WA SHULE TEULE ZA SEKONDARI WILAYANI NYAGATARE NCHINI RWANDA

Emilien Bisamaza
Chuo Kikuu cha Rwanda
bisamazamilien@gmail.com

*DOI: https://dx.doi.org/10.4314/jclfkt.v4i1.4*

**Ikisiri**

*Makala hii inabainisha nafasi ya hadithi katika kufundishia na kujifunzia stadi za kusikiliza na kuzungumza. Aidha, makala inalenga kuunda mwongozo wa kutumia hadithi kufundishia na kujifunzia stadi hizo. Ukusanyaji wa data ulifanywa kupitia ushuhudiaji, mahojiano na uchanganuzi wa matini. Walengwa wa utafiti walikuwa wanafunzi na walimu wa Kiswahili kutoka shule teule za sekondari katika wilaya ya Nyagatare. Data zilizokusanywa, zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Nadharia ya Utambuzi ndiyo iliyoongoza makala hii. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa hadithi ina nafasi muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hadithi huwavutia wanafunzi, wakawa na motisha ya kujifunza bila uchovu. Kutokana na changamoto zilizoshuhudiwa kuhusu utumiaji wa hadithi kufundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza, uliundwa mwongozo ambao unawasilisha mambo ya kuzingatia kwa kila hatua ya somo. Mapendekezo mbalimbali yametolewa kwa wadau mbalimbali ili kufanikisha uungaji mkono wa kutumia hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza kama stadi za msingi.*

## 1.0 Utangulizi

Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia mazungumzo au matendo katika kuwasilisha ujumbe fulani kwa watazamaji au wasikilizaji (Ndungo, 1991). Mazungumzo hayo yanaweza kuimbwa, kutendwa au kuzungumzwa. Wamitila (2003) anaongeza kuwa fasihi simulizi inatumiwa katika jamii kama njia ya kupashana maarifa yanayohusu utamaduni, historia, matamanio, na mtazamo wao.

Katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, fasihi hutoa modeli ya lugha. Fasihi huwapatia wanafunzi wanaojifunza lugha fursa nyingi za kuboresha uelewa wao wa kisintaksia, kipragmatiki, kiutamaduni na kiusemi. Pia, inawawezesha kuwa na umilisi wa stadi za lugha. Stadi hizo ni kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma. Hivyo basi, ufundishaji na ujifunzaji wa lugha unahitaji matumizi ya fasihi na ushirikishwaji wa matini ya kifasihi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza

stadi za kusoma, kuandika, kuzungumza, kusikiliza na tafakuri tunduizi (Shazu, 2014).

Kusikiliza na kuzungumza ni stadi za msingi ambazo hujenga haiba ya mwanafunzi. Hii inatokana na ukweli kwamba, stadi hizi ni muhimu kujenga uwezo wa mwanafunzi wa kuwasiliana na watu mbalimbali. Aidha, stadi za kusikiliza na kuzungumza zina mchango mkubwa kuzifanya stadi za kusoma na kuandika ziwe imara. Ujuzi wa stadi hizi unategemea mwalimu atumie muda wa kutosha na mbinu anuwai zinazomshirikisha mwanafunzi kutagusana na kuingiliana na wengine katika mazungumzo, michezo ya lugha, dayolojia, na mijadala inayohusu mazingira na miktadha inayoakisi hali halisi (Smith, 1995).

Prabhu (1987) akirejelewa na Rosemary (2010) anatoa maelezo kwamba kusikiliza na kuzungumza ni stadi zisizopewa umuhimu katika ufundishaji. Hivyo, mbinu zinazotumiwa kufundisha stadi hizo ni lazima ziwe zile zinazowapatia wanafunzi fursa na uwezo wa kutoa maelezo yao yanayohusisha miktadha tofauti ya mawasiliano. Kutokana na hayo, wanafunzi wanakuza uwezo wao wa kuzitumia dhana wanazofundishwa wakati mwalimu anapojumuisha mazoezi ya kimazungumzo katika ufundishaji wake. Mazoezi hayo ni kama vile kuzungumza katika makundi, kuigiza, kucheza michezo ya maneno na mazungumzo ya kimwingiliano na kimtagusano kama maamkizi, kumshukuru mtu, na kumuomba radhi (Ur, 1981).

Thamani ya ufundishaji wa kusikiliza na kuzungumza imejikita katika ukweli kwamba wanafunzi, hasa katika hatua zao za mwanzo za ujifunzaji lugha, wanaelewa kwa urahisi wanavyosikiliza kuliko wanavyosoma. Kwa njia ya kusikiliza hadithi, wanafunzi wanajifunua kwa eneo pana la uzoefu wa usikiaji unaowasaidia kuongeza maarifa yao ya uwezo wa lugha watakayofundishwa. Ingawa stadi ya kusikiliza ni mojawapo ya stadi za lugha, ndiyo stadi inayofundishwa kwa kiwango kidogo ukilinganisha na stadi nyingine za mawasiliano (Mousena, 2020). Stadi ya kusikiliza inashirikisha stadi za kuzungumza, kusoma na kuandika.

Hadithi ambacho ni kipera cha fasihi simulizi kinachukuliwa kama kipera kimojawapo kinachoweza kuwasaidia wanafunzi kukuza umilisi wa lugha. Hii inatokana na kwamba wanafunzi wanaozoea kusikiliza hadithi, ndio huwa wasikilizaji na wasimuliaji hodari. Na wasimuliaji hodari huwa pia watoa habari wa kuaminika (Piscayanti na Wedhanti, 2012). Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa wa kutumia hadithi kukuza stadi za lugha ambazo ni kusikiliza na kuzungumza kama stadi muhimu kwa mjifunzaji lugha. Ikumbukwe pia kwamba, stadi hizi hazipewi mkazo na watu wengi, wakiwamo walimu na wakaguzi. Mara nyingi wanatilia mkazo ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika, na kuacha zile za kusikiliza na kuzungumza (Ali, 2015).

Hivyo, makala hii inabainisha nafasi ya hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza na kuunda mwongozo wa kutumia hadithi katika kufundisha na kujifunza stadi za kusikiliza na kuzungumza.

## 2.0 Methodolojia ya Utafiti na Nadharia

Utafiti wetu ulitumia usanifu wa kitaamuli kukusanya data. Shule mbili za sekondari ziliteuliwa: G.S Gikagati, na G.S Rurenge. Shule hizi mbili zina mchepuo wa lugha ambapo lugha ya Kiswahili inafundishwa kama somo la kutathminiwa katika mtihani wa taifa. Wanafunzi wanaoshinda vizuri mitihani hii, huendelea na masomo yao katika vyuo.

Data zilikusanywa kwa kutumia njia ya mahojiano, ushuhudiaji na uchanganuzi wa matini. Wakati wa kukusanya data, mtafiti alishuhudia vipindi vinne vya masomo darasani. Vipindi viwili vilihusisha masomo ya kufundisha stadi ya kusikiliza, na viwili vya kufundisha stadi ya kuzungumza Kiswahili. Katika uchambuzi wa data, walengwa wa utafiti walipewa msimbo kutokana na shule walizotoka. Wanafunzi walipewa msimbo wa A. Kwa ajili ya kuwabainisha, tuliongeza tarakimu. Kwa hiyo, tulikuwa na A1 na A2 kwa wanafunzi wa shule ya kwanza, na A3 na A4 kwa wanafunzi wa shule ya pili. Walimu walioshiriki nao walipewa msimbo wa B. Ili kuwabainisha, tuliongeza tarakimu, na tulikuwa na B1 kwa mwalimu wa shule ya kwanza, na B2 kwa mwalimu wa shule ya pili.

Utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Utambuzi iliyoasisiwa na Piaget (1972). Nadharia hii inadai kuwa mzungumzaji wa lugha ana uwezo wa kubuni na kuelewa tungo kwa kuiga tu yaliyosemwa na wazungumzaji wengine. Nadharia ya Utambuzi ilifaa katika utafiti wetu kwa sababu inadokeza viambajengo vinavyorejelewa katika ufundishaji. Viambajengo husika ni pamoja na jukumu la mwalimu kama mwelekezaji, majukumu ya mwanafunzi katika usakaji wa maarifa, mazingira ya kufundishia na majukumu ya kushiriki kwa wanafunzi katika ujifunzaji. Licha ya nadharia hii kuwa na mihimili mingi, tuliona kwamba mihimili mitatu ndiyo inafaa kulingana na utafiti wetu.

Mhimili wa kwanza unasema kwamba mwanafunzi anapaswa kushirikishwa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili aweze kuzingatia yale anayofundishwa. Mwanafunzi ana jukumu la kuwa mshiriki hai katika yale anayofundishwa. Mhimili huu unaonesha wazi kwamba wanafunzi wanapaswa kushirikishwa katika utambaji wa hadithi ili waweze kukuza stadi zao za kusikiliza na kuzungumza. Mhimili wa pili unasisitiza umuhimu wa mwalimu kujenga mazingira ya ufundishaji. Mazingira haya yawe ya kumsaidia mwanafunzi kupata ufahamu na uelewa wa aliyofundishwa. Mhimili huu utatusaidia kuonesha namna mwalimu anavyopaswa kujenga mazingira ya ujifunzaji yanayowashirikisha wanafunzi katika ukuzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Mhimili wa tatu unasisitiza

kuwa ni lazima kuweka mkazo katika ufundishaji unaoanzia kwa kile kinachofahamika kwa mwanafunzi kwani ndio hurahisisha uwezo wa kiutambuzi. Mhimili huu utatusaidia kuonesha namna mwalimu anavyopaswa kuanzia kwa kile wanafunzi wanachojua ili aweze kukuza stadi husika kwa kikamilifu.

**3.0 Nafasi ya Hadithi Kukuza Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza**

Data za mahojiano zinaonesha kwamba wanafunzi wanaiona hadithi kuwa ina mchango muhimu katika kufundisha kusikiliza na kuzungumza. Haya yalithibitishwa na hoja zao zifuatazo:

> Tunapojifunza stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kutumia hadithi, tunapata ujumbe kwa urahisi. Pia, tunaweza kurudia tuliyosimuliwa kwa urahisi, kwa sababu masimulizi ya hadithi au kazi nyingine ya fasihi simulizi ni ya kusisimua na yanatufurahisha sana. Kwa hiyo, tunafuata kwa makini kabisa na tukajifunza lugha kwa urahisi (A1).

Dondoo hili linatuonesha kuwa hadithi ni mwafaka kufundishia na kujifunzia stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hii inasababishwa na kwamba hadithi wanayosimuliwa inawasaidia wanafunzi kupata ujumbe kwa urahisi kwa kuwa wana furaha na motisha ya kufuata kwa makini.
Mwanafunzi mwingine aliyehojiwa naye alithibitisha:

> Nina uhakika kwamba kazi za hadithi zinakuza uwezo wa mtu wa kusikiliza na kuzungumza. Wakati tunaposimuliwa hadithi na mwalimu darasani tunamtegea sikio ili tusikose habari yoyote inayosimuliwa. Tunavutiwa sana na namna hadithi zinavyopangwa, na namna zinavyohusisha vipengele vingine kama nyimbo, methali, na vinginevyo. Ndiyo sababu tunamsikiliza mwalimu kwa utulivu na kimya anapotusimulia hadithi. Kwa hiyo, tunafurahishwa na vitendo vya wahusika. Baadhi ya wanafunzi huwa na hisi tofauti. Kuna ambao hulia, huhuzunika, hushabikia, au huchukia baada ya kusimuliwa hadithi (A3).

Dondoo hili linatuonesha kuwa hadithi ni mwafaka kufundishia na kujifunzia stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hii inasababishwa na kwamba hadithi inawasaidia wanafunzi kupata ujumbe kwa urahisi. Maoni haya yanaendana na mmojawapo wa mihimili ya Nadharia ya Utambuzi ambao unasisitiza mwanafunzi ashirikishwe katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mchakato huo humwezesha kutambua kilichomo katika hadithi anazosimuliwa. Mwanafunzi ana uwezo wa ndani katika ung’amuaji wa mambo. Wanafunzi wanatambua waliyosikia na wanaweza kuyazungumza.

Hadithi huwasaidia wanafunzi kujifunza stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa urahisi. Kutokana na kusimuliwa, wasimuliwa nao wanakuza stadi yao ya

kusikiliza na kufahamu. Kwa hiyo, wasimuliwa nao wanapata umilisi wa kueleza na kuwasilisha hisia zao kwa wengine. Masimulizi ya hadithi yanasisimua wasikilizaji kwa kiwango cha kuwafanya kushiriki. Kwa mfano, msimuliaji akiwa anasimulia hadithi, kuna sehemu za hadithi zinazorudiwarudiwa. Sehemu hizi wasikilizaji wanazinasa kwa urahisi na wanamsaidia msimuliaji kuzisimulia. Hivyo, wasikilizaji hujizoeza kuzungumza bila hofu yoyote kwa kuwa wanazungumza yale waliyoyanasa. Mfano wa hadithi zilizo na sehemu inayoimbwa ni *Sultani Majinuni* katika Edward (1870). Mtoto anaimba, "*Mama wee, niulaga Nunda mla watu*." Mama yake akamjibu pia kwa kuimba, "*Mwanangu, si yeye Nunda mla watu*". Maelezo haya yanaendana na mmojawapo wa mihimili ya Nadharia ya Utambuzi unaosisitiza kuwa mwanafunzi anajifunza kuanzia kwa kile anachokifahamu. Mwanafunzi anapata na kuelewa anavyojifunza kutokana na malengo aliyojiandalia. Ufaafu wa kutambua ndio unamwelekeza mwanafunzi kufahamu habari alizojifunza kwa kutumia akili kutokana na matini anazozitumia. Kwa kusikiliza habari ya *Sultani Majinuni*, kwa mfano, mwanafunzi anafahamu kuwa si vizuri kukata tamaa unapotaka kutimiza lengo lako.

Hadithi zinahifadhi mambo yote yanayopatikana kwenye jamii. Mambo hayo ni pamoja na utamaduni, mila na desturi za jamii. Katika hadithi, tunakuta pia miiko, itikadi na mwelekeo wa jamii. Mambo haya yote, yanaelezwa kwa lugha rahisi na ya kusisimua kiasi kwamba kila mwanafunzi anaweza kuyaelewa. Mtafitiwa B2 anathibitisha hoja hii kwa kusema:

> Hadithi zina upekee wa kuvutia wanafunzi. Hii ni kutokana na visa na matukio pamoja na migogoro kati ya wahusika. Wanafunzi wanavutiwa na kusikiliza mtiririko wa matukio na visa, pamoja na mwingiliano wa vipera vingine kama methali, nahau, nyimbo… katika hadithi. Mara nyingi wanafunzi wanafuata kwa makini wakati tunapowasimulia hadithi kwa sababu wana hamu kubwa ya kujua namna mambo yalivyomalizika.

Ufundishaji na ujifunzaji wa kusikiliza na kuzungumza hurahisishwa kutokana na kutumia hadithi. Wanafunzi hupata urahisi, kwanza, wa kumsikiliza msimuliaji ambaye anawasimulia hadithi wanazofurahia. Pili, hupata urahisi wa kuzungumza kwa sababu baada ya kusikiliza hupewa fursa ya kuzungumza. Wanaweza kujibu maswali ya ufahamu waliyoulizwa na mwalimu. Aidha, wanafunzi wanaweza kutoa kwa njia ya mazungumzo muhtasari wa hadithi waliyosikiliza. Kwa ujumla, hadithi zinaleta motisha kubwa kwa wanafunzi na kuwafanya kuwa hai katika somo.

Kwa kusisitiza mawazo hayo ya nafasi ya hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza, Sywal (2015:7) anasema:

> *The students are actively response the story that is told by their friend* alternately *while the others propose or answer a question that is given*

> *by the lecturer or their friends. Besides that, they are also having enough self confidence in constructing and discussing the moral messages in the oral literacy. Through oral literature-based instruction, the students are able to stimulate important skill in speaking process that is ability in reconstructing imaginative story becomes easier to be understood.*
>
> Wanafunzi wanaitika kwa uhai hadithi iliyosimuliwa na rafiki yao kwa mbadala wakati ambapo wengine hupendekeza au hujibu swali lililotolewa na mwalimu au rafiki zao. Zaidi ya hayo, wanajiamini pia sana katika uundaji na ujadilianaji wa habari za maadili katika umilisi wa kimasimulizi. Kupitia mafunzo yanayoegemea fasihi simulizi, wanafunzi wanaweza kuchochea stadi muhimu katika mchakato wa kuzungumza. Ni kumaanisha kuwa uwezo katika ujenzi wa hadithi bunilizi unaeleweka kwa urahisi. [Tafsiri yetu]

Tunaunga mkono maelezo ya mtaalamu huyu. Wanafunzi hufurahia kusimuliwa hadithi au kazi nyingine ya fasihi simulizi. Kazi hizi zinawavutia na kuwafanya wawe hai katika somo. Hii inawasaidia kukuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Wanaposimuliwa hadithi, hawakuzi tu stadi yao ya kusikiliza, bali wanakuza pia uwezo wao wa kufikiria, kujenga maadili, na kuweza kuzungumza kwa ufasaha. Sywal (khj) anaendelea kwa kusema kwamba hadithi zinarahisisha usikilizaji na uzungumzaji:

> *Through oral story-based instruction, the students are able to express uniqness and introduce one of their cultures to the other students which are come from different place. Speaking is a process of transferring knowledge which is originate from oneself, expressing emotion, experience, thinking and self-imagination in order that the speaking ability is not only as an activity to improve speaking ability … but also as activity to improve emotion, imagination and critical ability.*
>
> Kupitia mafunzo yaliyoegemea katika hadithi simulizi, wanafunzi wana uwezo wa kueleza upekee na kuwasilisha moja ya tamaduni zao kwa wanafunzi wengine wanaotoka katika sehemu tofauti. Uzungumzaji ni mchakato wa kuhamisha maarifa yanayotoka kwa mtu mwenyewe, akieleza hisia, uzoefu, fikra na ubunifu wake ili uwezo wa kuzungumza usiwe tu zoezi la kuendeleza umilisi wa kuzungumza pekee…, bali uwe pia zoezi la kukuza hisia, ubunifu na uwezo wa kihakiki. [Tafsiri yetu]

Tunakubaliana na maoni ya mtaalamu huyu kuhusu nafasi ya hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Kutokana na hadithi, mwanafunzi ana uwezo wa kujieleza kihisia na kiutamaduni. Mwanafunzi

anaweza kuelezea utamaduni wake kwa wengine, hivyo ikawasaidia kushirikiana na kujiunga katika masomo yao.

Hadithi haikuzi uwezo wa kusikiliza na kuzungumza tu, bali inakuza pia uwezo wa kufikiria, kubuni, kuwa na uzoefu katika maisha, na kuwa na uwezo wa kuhakiki. Mwanafunzi anapojifunza kupitia hadithi, anaendeleza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Isitoshe, anakuza pia uwezo wake wa kutoa hisia zake, kuhakiki kazi alizozisikiliza, kubuni kazi nyingine, na kupanua uwezo wake wa kufikiria. Maelezo haya yanaendana na mmojawapo wa mihimili ya Nadharia ya Utambuzi unaoeleza kwamba, mkazo huwekwa katika ufundishaji unaoanzia katika kile kinachofahamika kwa mwanafunzi kwani ndio hurahisisha uwezo wa kiutambuzi. Kujiendeleza kiutambuzi huhitaji mwanafunzi aweze kuwa na tafakuri, suluhisho la matatizo na uwezo wa kutumia lugha. Kwa mfano, mwanafunzi anaposikiliza hadithi ya '*Mfalme Chura*', anaweza kutafakari na kujua kuwa kila mtu ni muhimu na anaweza kusaidia katika hali fulani. Aidha, kila mtu awe na utu kwa wote na kwa viumbe vyote.

Hadithi ina nafasi kubwa katika ufundishaji wa stadi hizi za msingi ambazo ni kusikiliza na kuzungumza. Hadithi hurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi hizi mbili, kwa kuwa zinawavutia wanafunzi na kuwafanya kuwa na motisha ya kusikiliza. Aidha, hadithi zinawasisimua wanafunzi wanapojifunza, na kuwawezesha kuzungumza bila uoga mbele ya hadhira kwa kutumia lugha sanifu na fasaha tofauti na lugha wanayotumia katika mazungumzo ya kawaida.

## 4.0 Hali ya Ufundishaji wa Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza kwa Kutumia Hadithi

Ingawa walimu wanaona kuwa hadithi ina nafasi muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza, wana changamoto ya kujumuisha hadithi katika hatua zote za somo. Kutokana na data za ushuhudiaji, ilionekana kuwa walimu wanapofundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza, katika maandalizi yao ya somo, na wakati wa kufundisha, wana changamoto ya kujumuisha hadithi. Katika ushuhudiaji na mahojiano na walimu, maoni tofauti kuhusu kutojumuisha hadithi katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza yalitolewa. Akitoa maoni kuhusu hoja hii, mtafitiwa B1 anasema:

> Kutokana na ratiba tunayotumia, pamoja na vitabu vya Kiswahili tunavyotumia, stadi za kusikiliza na kuzungumza zinakuja baada ya kipindi cha matumizi ya lugha. Katika vitabu tunapatiwa mada ya kujadili tu. Kwa hiyo, tunafuata maandalizi hayo ya vitabu vya Kiswahili. Tunahitaji kusaidiwa na kuwa na nia ya kutumia hadithi katika ufundishaji wa kusikiliza na kuzungumza.

Dondoo hili linaeleza wazi kuwa hadithi haihusishwi katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Walimu hufuata mfumo wa vitabu wanavyotumia.

Wanaonesha kuwa kutumia hadithi kufundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza ni muhimu sana na vitasaidia wanafunzi kukuza stadi hizi kwa kiasi kikubwa. Hoja hii inatiliwa nguvu na mtafitiwa B2 ambaye anasema:

> Tunaona kuwa hadithi ina nafasi kubwa kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Lakini tumezoea kutumia midahalo na mijadala tu, tunapofundisha stadi hizi. Kwa hiyo, ni lazima tubadilishe namna tulivyokuwa tunafundisha stadi hizi, tuanze kujumuisha hadithi katika ufundishaji wa kusikiliza na kuzungumza.

Dondoo hili linaonesha utashi wa walimu wa kutumia hadithi kufundisha na kujifunza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Walimu wanaona kuwa hadithi ikijumuishwa, itarahisisha ufundishaji wa stadi hizo. Kwa hiyo, mwongozo wa kutumia hadithi kufundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza, uliundwa ili kutatua tatizo la kutojumuisha hadithi katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza.

## 5.0 Mwongozo wa Kutumia Hadithi Kufundisha na Kujifunza Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza

Kutokana na maudhui yaliyojadiliwa katika sehemu iliyopita, kutokana pia na nafasi ya hadithi kufundishia stadi za kusikiliza na kuzungumza, na kutokana na data za ushuhudiaji, tumeona kwamba ni bora kutoa mwongozo unaoweza kufuatwa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwongozo ni kanuni za msingi za kufuata kufanya jambo fulani. Katika makala hii, mwongozo unahusisha mambo ya kuzingatia katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kutumia hadithi. Mwalimu anapaswa kuzingatia mambo hayo katika sehemu tatu zinazohusiana na somo lake kwa ujumla. Sehemu hizo ni: andalio la somo, ufundishaji wa somo na tathmini ya somo.

### 5.1 Mwongozo Kuhusu Andalio la Somo kwa Kujumuisha Hadithi

Kutumia hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza kunahitaji maandalizi na mafunzo yanayojiegemeza katika hadithi. Mwalimu anapofundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza, anapaswa kuhakikisha kwamba malengo yake ya somo yanajumuisha hadithi. Kwanza, wakati wa kuandaa malengo ya ujifunzaji yanayotarajiwa katika somo la stadi za kusikiliza na kuzungumza, mwalimu anapaswa kujumuisha hadithi ili aweze kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi hizi. Kwa mfano, anaweza kuandika: kwa kutumia hadithi ya *Yai la Dhahabu*, wanafunzi wataweza kusikiliza na kutoa muhtasari wa hadithi hiyo katika mazungumzo. Pili, anapaswa kuhakikisha kwamba katika hatua ya kufundisha kusikiliza na kuzungumza, ana hadithi ya kuwasimulia wanafunzi. Anaweza kuisimulia mwenyewe au iwe imerekodiwa. Tatu, ahakikishe kuwa muktadha wa darasani utawasaidia wanafunzi kusikiliza bila pingamizi.

Nadharia ya Utambuzi inasisitiza haya kutokana na mmoja wa mihimili yake usemao kuwa wajibu wa mwalimu ni kutayarisha mazingira ya kurahisisha namna wanafunzi wanavyojifunza. Hii inawawezesha kuelewa na kufahamu yale ambayo yangekuwa magumu kwa juhudi zao binafsi.

**5.2 Mwongozo Kuhusu Ufundishaji wa Somo kwa Kutumia Hadithi**

Wakati wa kuwasilisha somo, mwalimu anapaswa kuwashirikisha wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji, kisha akawasimulia hadithi aliyoandaa. Wanafunzi wanapewa mafunzo ya kuisikiliza kwa utulivu na makini. Mwalimu kama mwelekezaji, anapaswa kuhakikisha kwamba wanafunzi wote darasani wanasaidiwa kusikiliza hadithi. Baada ya kusikiliza hadithi, mwalimu anatoa mazoezi ya kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anafuata. Mazoezi hayo ni pamoja na maswali ya ufahamu wa hadithi pamoja na muhtasari wake kimazungumzo. Hii inaendana na maelezo ya Kegan (1982) kuhusu mhimili wa Nadharia ya Utambuzi. Kegan (khj) anasema kwamba, majukumu ya mwalimu ni pamoja na kushirikisha wanafunzi katika ufundishaji. Kwa hiyo, mwalimu ana jukumu la kujua kiwango cha uwezo wa utambuzi wa wanafunzi na kubadilisha mbinu na zana za kufundishia, ili kuona kuwa kubadilisha huko kutaleta mchango utakaofanikisha ufundishaji.

Mwalimu huwasaidia wanafunzi kusikiliza, na kusimulia hadithi. Mwalimu anatumia mbinu tofauti zinazowawezesha wanafunzi kuwa na umilisi wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Umilisi huu utawasaidia wanafunzi kuwa wasimuliaji wazuri wa hadithi na wasikilizaji wazuri kwa ujumla. Kuhusu namna mwalimu anavyoweza kufundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kutumia mbinu tofauti, Ildrimzade (2018:40) anasisitiza:

> *…dramatization, improvisation, role*-*playing, pantomiming, reenactment,* discussion*, and group activities may center on a work of literature. The most heard discourse is more spontaneous, lacks formal words, and contains taboo words and other expressions that are typical in spoken language. The next point about listening is that it is a reciprocal skill. It is said that listening cannot be practiced in the same way as speaking. Listening involves a variety of skills and the process of listening in face-to-face conversation includes specific elements: the spoken signals have to be identified, the speech has to be segmented into parts (which have to be organized), the speaker's intended meaning should be understood, the speakers' and listeners' knowledge of syntax and grammar is needed. Due to these listening skills, we can say that they do not occur separately but happen at the same time of speech. In the field of literature, few types of listening exercises are suggested – listening to an audiocassette, listening to teacher as a storyteller, listening to a role-play etc.*

> … Uigizaji, umithilishaji, , uigizaji wa kutumia ishara, ufananishaji, mjadala, na kazi za makundi huweza kulenga hadithi. Masimulizi yanayosikilizwa sana ni ya papo kwa papo, yanakosa maneno rasmi, yanasheheni maneno ya miiko, na maneno mengine ya kawaida yanayotumiwa katika lugha ya kimazungumzo. Inasemwa kuwa stadi ya kusikiliza haiwezi kuwekwa katika vitendo kwa namna sawa na stadi ya kuzungumza. Usikilizaji unahusisha stadi anuwai, na mchakato wa usikilizaji katika mazungumzo ya ana kwa ana unatia ndani elementi maalumu: ishara zilizozungumzwa lazima zibainishwe, usemi ugawanywe katika sehemu (ambazo zinapaswa kuundwa), maana iliyotarajiwa na mzungumzaji ieleweke. Mzungumzaji na msikilizaji wanahitaji kuwa na ujuzi wa sintaksia na sarufi. Kutokana na stadi hizi za usikilizaji, tunaweza kusema kuwa hazitokei zikitenganishwa, bali zinatokea kwa wakati mmoja wa usemi. Katika hadithi, aina chache za mazoezi ya usikilizaji zimependekezwa: kusikiliza kaseti ya sauti, kusikiliza mwalimu kama msimuliaji wa hadithi, kusikiliza uigizaji na kadhalika. [Tafsiri yetu]

Kutokana na dondoo hili, tunahimiza walimu kutumia hadithi wakati wanapofundisha. Mwalimu azitumie mbinu kama vile uigizaji, kucheza nafasi, na ufananishaji wakati wa kufundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza kupitia hadithi. Hii inatokana na kwamba, kwa kawaida, mwalimu ndiye mdhibiti wa ufundishaji. Anapaswa kuteua mbinu anayoona kwamba itafaa kwa somo lake na kuamua mkondo ambao somo hilo litachukua.

Mwalimu anahimizwa kuorodhesha hadithi zinazoegemea katika mtaala anaoutumia na kuzitumia zile zilizoandikwa vitabuni au la. Aidha, anapaswa kuhakikisha kwamba hadithi anazozichagua zinawashirikisha wanafunzi katika somo na kumsaidia kufika kwenye malengo ya somo yanayotarajiwa. Hii inatokana na kwamba njia nzuri ya kufundisha ni ile inayomwezesha mwalimu kutimiza madhumuni ya somo, inayowavutia wanafunzi, inayodokeza mazoezi ya kuwasaidia wanafunzi kulielewa somo, isiyowachosha walimu na wanafunzi bali inayowawezesha kufikia matarajio yao. Kwa hivyo, hadithi zina nafasi muhimu katika kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza.

Wakati wa kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza kupitia hadithi, mwalimu pia anapaswa kuweka mkazo kwenye mazoezi anayotoa kutokana na hadithi iliyosimuliwa. Mazoezi hayo ni kama vile kuzungumza kwenye makundi, kuigiza katika miktadha mbalimbali ya kimawasiliano, kucheza michezo ya maneno ya lugha yanayotoka katika hadithi na kutumia mazungumzo ya kimwingiliano kama maamkizi, kumuomba radhi mtu, na kumshukuru. Njia nyingine zinazoweza kutumiwa ni kama uigizaji wa hadithi waliyosimuliwa, kucheza nafasi, mdahalo na mjadala kwa mada inayohusiana na hadithi.

Mwanafunzi huchukuliwa kama mhusika anayeshiriki kwa upana katika ufundishaji (Ur, 1981).

Wanafunzi wanapaswa kushirikishwa kikamilifu katika somo la masimulizi ya hadithi. Hii ni kwa sababu mbinu za ufundishaji zinazofaa katika mchakato wa ujifunzaji hai ni zile zinazoweka mkazo katika ushiriki mkubwa wa mwanafunzi, mwalimu akawa mwelekezaji.

**5.3 Mwongozo Kuhusu Tathmini**

Wakati wa kutathmini, mwalimu asimulie wanafunzi hadithi darasani au wanafunzi wasimulie wanafunzi wengine hadithi wanayojua. Kitendo hiki kinapomalizika, mwalimu awaweke wanafunzi katika makundi ili waweze kujadiliana na kufanya muhtasari wa mambo waliyoyasikiliza. Hii inawapa fursa wanafunzi kujadiliana kati yao, na kila mmoja anafanya ufupisho wake na kuuwasilisha mbele ya wengine. Wakati wa kuwasilisha, mwanafunzi anaweza kujibu maswali anayoulizwa na wenzake. Kupitia mawasilisho na kujibu maswali, mwanafunzi anapata fursa ya kukuza stadi zake za kusikiliza na kuzungumza, na hivyo kukuza umilisi wa kuzungumza mbele ya watu wengine bila woga. Hadithi zinazosikilizwa zinapaswa kuzingatia miktadha ya kimawasiliano inayopatikana katika mazingira ya mwanafunzi. Mwalimu naye atumie hadithi zenye miktadha inayozingatia mambo halisi yanayolingana na maisha ya wanafunzi. Mazoezi ya kusikiliza ni kichocheo kwa mwanafunzi cha kutafakari masimulizi ya hadithi anayoyasikiliza.

Zaidi ya kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza, mazoezi ya kusimuliwa hadithi yana pia lengo la kuimarisha uelewa wa miundo ya lugha na yenye mvuto na maarifa anayoyahitaji mwanafunzi (Rosemary, 2010). Ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza kutumia hadithi unapaswa kuwa na malengo dhahiri na yanayoweza kupimika.

Wakati wa kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza, ni muhimu kuwapa wanafunzi muda wa kutosha wa kusikiliza hadithi inayosimuliwa ili waweze kuwa na umahiri wa kusikiliza, na kusimulia walichosikiliza katika hadithi. Hii inatokana na kwamba umahiri wa kusikiliza na kuzungumza unatokana na mazoezi mengi ya kusikiliza na kuzungumza katika mazingira anuwai ya kimwingiliano. Hadithi zinazingatia miktadha ya kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza, kusikiliza na kudadisi.

Kwa ujumla, wakati wa kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kutumia hadithi, mwalimu anapaswa kuwasimulia wanafunzi kazi za hadithi alizoteua, na kuwashirikisha wanafunzi katika usikilizaji, kujibu maswali ya ufahamu na kutoa muhtasari wa kimazungumzo kuhusu hadithi walizosimuliwa. Mwalimu pia anaweza kuwaomba wanafunzi kusimulia hadithi, kutega vitendawili, kutoa muhtasari kwa kutumia methali, na kadhalika. Mwalimu

anapaswa kujumuisha hadithi na kuwashirikisha wanafunzi katika somo na katika kila hatua ya somo. Mwalimu kama mwelekezaji wa wanafunzi ndiye anawaelekeza kutenda yaliyoandaliwa.

## 6.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii imeshughulikia nafasi ya hadithi katika kufundisha na kujifunza stadi za kusikiliza na kuzungumza katika shule teule za sekondari wilayani Nyagatare. Lengo lake ni kubainisha nafasi ya hadithi na kuunda mwongozo wa kutumia hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hadithi ina nafasi muhimu katika kufundishia na kujifunzia stadi za kusikiliza na kuzungumza. Wanafunzi huvutiwa na masimulizi ya hadithi na humfuatilia kwa makini mwalimu anayewasimulia hadithi. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa nafasi ya hadithi kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza ni kubwa sana.

Kwa kawaida, hadithi huzingatia miktadha anuwai ya maisha ya jamii inayotumia fasihi simulizi. Katika hadithi, wanafunzi wanajifunza utamaduni, mila na desturi za jamii inayohusika. Pia, wanafunzi huvutiwa na masimulizi, mtiririko wa visa na matukio, na migogoro ya wahusika wa hadithi. Kwa hiyo, nafasi ya hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza ni kubwa na ni ya lazima. Lengo la pili la kuunda mwongozo wa kutumia hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza nalo limetimizwa. Mwongozo huo umeundwa, ambapo walimu wa sekondari hawana budi kuutumia katika ufundishaji wa stadi hizi. Mwongozo huo unazingatia ushiriki wa mwanafunzi katika hatua za kufundisha na kujifunza, na mwalimu akawa mwelekezaji.

Makala hii inatoa mapendekezo mbalimbali kwa walimu, Wizara ya Elimu na wakuza mitaala na kwa tafiti zijazo, ili hadithi itumiwe katika kufundishia na kujifunzia stadi za kusikiliza na kuzungumza. Mosi, walimu wanapaswa kutumia hadithi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Walimu wazingatie mwongozo wa kutumia hadithi katika kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Pia, walimu watafute hadithi za kutosha ili waweze kuchagua hadithi zinazofaa kulingana na matarajio na uelewa wa wanafunzi. Aidha, walimu watayarishe zana na vifaa vinavyoweza kuwasaidia kusimulia hadithi walizoteua. Vifaa hivyo ni kama vile matini za fasihi simulizi, zana za kisasa kama redio, televisheni, filamu, vinasasauti na zana nyingine za teknolojia ya kisasa.

Pili, tunapendekeza Wizara ya Elimu kushughulikia matini ya hadithi na vifaa vya kutumia katika masimulizi ya hadithi na kuvigawa kwa njia ya usawa katika shule za sekondari katika nchi ya Rwanda ili kukuza na kuendeleza stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kutumia hadithi. Wakuzamitaala watilie maanani ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Ni jambo muhimu wakuzamitaala kutilia mkazo kwenye mbinu za ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza.

Pia, washughulikie mwongozo wa kutumia hadithi kufundisha na kujifunza stadi za kusikiliza na kuzungumza.

Tatu, kuna haja kubwa kwa watafiti kutafiti kuhusu nafasi ya hadithi katika ufundishaji wa stadi nyingine ambazo si stadi za kusikiliza na kuzungumza. Utafiti ufanywe kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za mawasiliano katika maeneo mengine ya nchi. Tafiti hizo zinaweza kulingana na utafiti huu, lakini ziwe zinatafiti zaidi ufundishaji wa stadi nyingine za mawasiliano zisizohusishwa katika utafiti huu. Aidha, utafiti unaweza kufanywa kuhusu fasihi simulizi katika ufundishaji wa lugha kwa ujumla, na kwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili.

**Marejeleo**

Ali, L., H. (2015). *Changamoto na Mbinu za Kiisimu katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Awali*. Tasnifu Iliyowasilishwa Kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Edward, S. (1870). *Hekaya za Waswahili kama Zilivyosimuliwa na Wazawa wa Zanzibar*. Reedsy

Ildrimzade, L. J. (2018). The Role of Literature in Teaching and Learning Language Skills.W*orld Science*, *3*(31), 39-41.

Kegan, N. (1982). *The Evolving Self: Problems and Processes in Human Development*. Masachusettes: Harvard University Press.

Mousena, E. (2020). Listening and Speaking as Powerful Literacy Practices. *Journal of the University of Patras UNESCO Chair, 7*(2), 17-26.

Ndungo, C., M. (1991). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Naroibi: Nairobi University Press.

Piaget, J. (1972). Development and Learning. In Lavatellic S. & Stendler F. (wah) (1972) *Reading in Child Behaviour and Development.* New York: Hacourt Brace.

Piscayanti, K., S., & Wedhanti, N., K. (2012). Pengaruh Pembelajaran Berbasis Sastra Lokal

Bali Terhadap Prestasi Menulis Naratif Bahasa Inggris, *Jurnal Pendidikan dan Pengajaran*, *45*(2),161-168.

Prabhu, N., S. (1987). *Secondary Language Pedagogy: A Perspective*. Oxford: Oxford University Press.

Rosemary, A., A. (2010) *Matumizi ya Mbinu ya Kimuktadha katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili katika Shule za Upili za Wilaya ya Kakamega.* Tasnifu iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Cha Masinde Muliro (Haijachapishwa).

Shazu, R., I. (2014). Use of Literature in Language Teaching and Learning: A Critical Assessment. *Journal of Education and Practice, 5*(7), 29-35

Smith, V. (1995). Hearing.In O. Hargie (mha), *Communication skills.* Athens Greek: Sextant.

Sywal, S. (2015). *The Effectiveness of Oral Literature-Based Intruction on Students'Speaking Ability*.Iliyosomwa tarehe 06/08/2021 kutoka https://www.researchgate.net/publication/315671195

Ur, P. (1981). *What is in a Word?* Cambridge: Cambridge University Press.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd